

(١)

Wema kwa Mama ni njia ya Baraka Duniani na Rehma huko
Akhera.
Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu {Na tumemuuusia mwanadamu kwa Wazazi wake wawili, Mama yake aliubeba ujauzito wake kwa tabu juu ya tabu, na kumnyonyesha kwa miaka miwili, ni kwamba nishukuru mimi na Wazazi wako wawili na kwangu ni marejeo yenu}.

Na ninashuhudia kwamba hakuna Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu, yeye pekee asiye na mshirika wake, na ninashuhudia kwamba Bwana wetu Muhammad ni Mja na ni Mtume wake. Ewe Mola wetu msalie na umrehemu na umbariki Mtume wetu, na Ali zake, na Maswahaba wake na atakayeufuata mwongozo wake kwa wema mpaka Siku ya Mwisho.

Na baada ya Utangulizi huu.

Hakika Wema ni jina linalokusanya mambo yote mazuri, na sifa njema, na maadili mema yanayorithisha utulivu katika nafsi, na kueneza upendo baina ya watu. Na huleta utulivu katika jamii zote. Na Mtume S.A.W, alipoulizwa kuhusu Wema akajibu: Wema ni Maadili Mema.

Na katika mambo yasiyo kuwa na shaka ndani yake ni kwamba Wazazi wawili wao ni watu wenye haki zaidi ya kutendewa wema katika watu. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuamrisha tuwafanyie wema Wazazi wawili, na tuwatendee mazuri, na kuwa na huruma kwao. Na tunapokiangalia Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, na katika Sunna za Mtume wetu S.A.W, tunaona jinsi unavyokuwa uhusiano wa juu baina ya

(۲)

watoto na wazazi. Ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yejote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa heshima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni.

Na Mtume S.A.W alikwishabainisha kwamba wema kwa wazazi wawili na kuwatekelezea haki zao ni katika Matendo bora mmo baada ya Swala ambayo ni Nguzo ya Dini na ni katika Misingi Kikuu ya Uislamu. Na Mtume S.A.W, alipouliizwa: ni kazi gani inayopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu? Akajibu kwa kusema: Ni Swala katika Wakati wake. Ikasemwa kisha nini? Akasema kisha kuwatendea wema wazazi wawili. Ikaulizwa kisha nini? Akasema kisha kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na hakika Uislamu umekiinua cheo cha Wema kwa wazazi wawili na kuwatendea mazuri, pamoja na kuwatunza, kisha Uislamu ukamuhusisha Mama zaidi kwa Wema na MAtunzo pamoja na Kumjali zaidi. Na kuna Mtu mmoja alienda kwa Mtume S.A.W, akasema: Ewe Mtume Wa Mwenyezi Mungu, ni nani mwenye haki zaidi ya mimi kuwa nae (kwa maana ya kumtendea wema zaidi)? Mtume akamwambia: Mama yako. Akauliza: Kisha nani? Mtuke akamjibu na kumwambia: kisha Mama yako. Akasema Yule Mtu: kisha nani? Mtume akamjibu na kumwambia kisha Mama yako. Akauliza tena: Kisha nani? Mtume akamwambia: Kisha baba yako. Na kutoka kwa Bi Aisha R.A, amesema: Nilimuuliza Mtume S.A.W: ni nani mwenyi haki ya juu zaidi kwa Mwanamke? Mtume S.A.W akamjibu na kumwambia: Ni Mume wake. Nikasema: ni watu gani wenye haki zaidi kwa mwanaume? Akasema Mtume S.A.W: Mama yake.

(۳)

Na hakuna cha kushangaza katika jambo hili, kama mama hana haki hii ya kimalezi, ni nani mwingine wa kuwa nayo? Ni nani mwenye haki ya kutekelezewa haki yake kuliko yule aliyekubeba tumboni mwake miezi tisa ambayo inalingana na miaka tisa?

Wakati akjifungua ujauzito wako, alikumbana na uchungu mkubwa, na akakunyonyesha maziwa yake, na anakuosha uchafu kwa mkono wake wa kuume, na akakupendelea kuliko nafsi yake katika chakula, na kwamba kidole chako kinapoumwa au malalamiko yaliyojitokeza mwishoni katika hali ya kusikitisha

Na kama angeliambiwa achague baina ya uhai wako na mauti yake, basi angechagua maisha yako kwa sauti ya juu. Ni nani mwenye haki ya kutendewa wema kuliko Yule ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuusia katika kauli yake pale aliposema: Na tumemuusia mwanadamu kwa wazazi wake wawili kuwafanya wema. Mama yake alimbeba tumboni mwake kwa uzito juu ya uzito, na akamzaa kwa uzito, kisha akambeba na kumlea kwa muda wa miezo thelathini.

Hakika katika Fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mja wake ni kumuwafikisha katika kuwatendea wema wazazi wawili na hasa hasa mama. Na yoyote atakayeongozwa katika hili basi atakuwa MWenyezi Mungu Mtukufu amempeleka katika kheri kubwa mno, na fadhila kubwa sana; ataziona athari zake, Baraka na kuwafikishwa na kunyooshewa mambo yake hapa Duniani, na anatarajia thawabu zake Mwenyezi Mungu, rehma na msamaha, pamjoa na uokovu wa siku ya Mwisho. Hakika kumtendea wema mama ni katika fadhila kubwa na matunda anayoyavuna mja kwa ajili ya Dunia na Akhera, na mionganini mwayo ni:

Kufanikiwa katika haja zake, na kuondoshewa mazito, na kupokelewa maombi yake. Na kutoka kwa Bin Omar R,A, kutoka kwa Mtume S.A.W, amesema: wakati watu watatu

(ε)

walipokuwa wakitembea walinyeeshewa na mvua, na wakakimbilia pangoni katika Jabali, kisha lango la pango likawafungia humo, wakaanza kusemeshana wao kwa wao: Hebu angalieni matendo mema mliyoyatenda kwa ajili ya mwenyezi mungu, kisha mumuombe kwa matendo hayo huwenda akakuondosheeni tatizo lenu. Mmoja wao akasema: Ewe Mola wangu hakika mimi nilikuwa na wazazi wawili vikongwe, na watoto wadogo, nilikuwa ninachinga mifugo kwa ajili yao, na nilikuwa nikiwaendea hukamua maziwa na nikawa nikianza kuwanywesha wazazi wangu kabla ya watoto wangu, na mimi siku moja nikachelewa na si kwenda mpaka ilipofika jioni, nikawaendea na nikawakuta wamelala, nikakamua maziwa kama nifanyavyo, na kusimama upande wa vichwa vyao nikichukizwa na kuwaamsha, na nikichukizwa pia na kuwanywesha wanangu kabla ya wazazi wangu wawili, huku watoto wakilia njaa miguuni kwangu mpaka palipokucha. Na ikiwa unajua kwamba mimi nilifanya vile kwa kutaka rehma zako Ewe Mola wangu, basi tufungulie sisi pango hili kidogo tuweze kuona mbingu, basi Mwenyezi Mungu akalifungua pango lile kidogo na wao wakaiona mbigu..., kisha kila mmoja wao akamwomba Mola wake kwa kazi yake aliyoifanya kwa nia safi na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu basi mwenyezi Mungu akawafungulia hali yao ya dhiki na shida waliyokuwa nayo. Na wakaja watu wengi kutoka Yemeni wakimjia Bwana Wetu Omar bin Khatwaab R.A. akawauliza: je nyinyi mko na Uweisu bin Aamir? Mpaka alipomfikia Uweisu akasema: je Wewe ni Uweisu bin Aamir? Akasema: Ndio mimi. Kutoka Muraad kisha kutoka Karnu? Akasema ndio. Omar akasema: Wewe ulikuwa na ugonjwa na mbaranga kisha ukapona isipokuwa sehemu ya dirhamu moja? Akasema: ndio. Akasema: je una mzazi wa kike?

(5)

Akasema: ndio. Akasema: nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: atakujieni Uweis bin Aamir akiwa na misafara ya mizigo ya watu wa Yemen kutoka Muraad yake mama hiyo kwa mama yako ni wema, kama ningeliapa mwa kwenye, na kama angeliapia kwa Mwenyezi Mungu angemwepusha.

Kisha kutoka Karan, alikuwa na mbaranga na akapona, ispuokuwa sehemu ya Dirhamu moja na ana mzazi wa kike na yeye anamfanyia wema, na kama ataigawa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi atamponya, kwa hiyo kama unaweza ukitaka akuombee msamaha basi fanya hivyo, niombee mimi msamaha, akamwombea msamaha, akamwambia Bwana wetu Omar R.A, unakusudia kwenda wapi? Akasema ninakusudia mwenda Kofa, akasema: Je nikuandikie kwa mtumishi wake? Akasema: mimi kuwa kwa watu wa chini ni bora kwangu, kwani katika maneno ya Mtume S.A.W, kuna ishara ya kuwa Mwenyezi Mungu amemkubalia dua yake kwa sababu ya kumtendea wema mama yake.

Ukubwa wa malipo na thawabu: na kutoka kwa Muawiya Salmiy anasema: nilimwendea Mtume S.A.W, nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi nilikuwa ninataka kwenda katika Jihadi pamoja na wewe nikitafuta kwa jambo hili radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo yake, akasema: Ole wako, Je Mama yako yuko hai? Akasema ndio. Akasema: Rejea kwa Mama yako na umtendee wema, kisha nikamjia kwa upande mwingine nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, mimi nilikuwa ninataka Jihadi kwa ahili ya radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo yake, akasema: Ole wako. Je una mama? Nikajibu ndio Ewe Mtume wa MWenyezi Mungu. Akasema: Rejea ukamtendee wema Mama yako. Kwani hiyo ndio Pepo yako.

(1)

Na kutoka kwa Kaab bin Ujrah R.A, ni kuwa Mtu mmoja alipitia kwa Mtume S.A.W, na Maswahaba wa Mtume S.A.W, waliiona ngozi yake na uchangamfu wake na kuwastaajabisha, wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu: Unaonaje kama hali hii ingekuwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu! Mtume S.A.W akasema: Ikiwa mtu huyu anachokihangaikia ni wanae wadogo basi hiyo ni katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Na ikiwa ametoka kwa ajili ya kuwahangaikia wazazi wake wawili waliozeeka, basi hiko ni katika Njia ya Mwenyezi Mungu.

Kusamehewa madhambi na makosa mbali mbali. na kutoka kwa Bin Omar R.A, ni kwamba kuna mtu mmoja alienda kwa Mtume S.A.W, akasema: Ewe Mtume wa MWenyezi Mungu, hakika mimi nimefanya dhambi kubwa mno, na je ninaweza kuomba toba? Mtume akasema: Je wewe una Mama? Akasema: hapana: akasema Mtume: Je wewe una mama mdogo? Akasema Mtume S.A.W, basi mfanyie wema.

Kufuzu Pepo mbali mbali, na kuwa katika daraja za juu. Na kutoka kwa Abdillahi bin Masoud R.A.amesema: Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni matendo yapi yanayomkurubisha mtu na pepo? Akasema: Ni swala katika nyakati zake. Nikasema: na nini kingine ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: ni kuwatendea wema wazazi wawili. Na kutoka kwa Bi Aisha R,A, amesema: Mtume S.A.W amesema: Nililala nikajioni nikiwa Peponi, na nikaisikia sauti ya msomaji akisoma, na nikasema: Ni nani huyu? Wakasema: Huyu ni Haarithah bin Nuumaan. Mtume S.A.W akasema: vivyo hivyo inavyokuwa kwa kutenda wema, vivyo hivyo inavyokuwa kwa kutenda wema. Na Harithah alikuwa mtu mwema mno kwa Mama yake miongoni mwa watu wema kwa wazazi wao.

(Y)

Kwa hiyo sisi tuwe ni wenyewe kuwafanya wema watoto wetu na mama zetu, tuwe ni wenyewe kuwatekelezea haki zao zote na tuwe na yakini kuwa kuwatendea wema wazazi wawili ni deni na kuwatendea uovu pia ni deni, na kama unavyomtendea mtu na wewe utatendewa. Hakika kuwatendea uovu wazazi wawili ni katika mambo ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameyafanya kuwa na adhabu Duniani na kesho, kwa kusadikisha kauli ya Mtume S.A.W, aliposema: Mambo mawili, Mwenyezi Mungu Mtukufu huyaharakisha. Upitukaji mipaka, na kuwatendea uovu wazazi wawili. Na katika Hadithi nyingine ya Mtume S.A.W: Hawezi kuingia peponi Mtu mwenye kuwatendea uovu wazazi wake wawili, au mwenye kuwasema aliyewasaidia, au mlevi aliye na uraibu wa pombe.

Ninaisema kauli yangu hii na ni

* * *

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, na rehma na amani zimfikie Bwana wa viumbe vyote, Rehma za Mwenyezi Mungu, Amani na Baraka zake zimfikie, na Watu wake, na Maswahaba wake wote, na yoyote atakayeufuata mwongozo wake kwa Wema mpaka siku ya Mwisho.

Enyi ndugu zangu waislamu:

Hakika kuwatendea wema wazazi wawili - na hasa mama - ni Jambo ambalo Sheria zote za Mwenyezi Mungu Mtukufu zimekubaliana, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na tulipochukua ahadi ya Kizazi cha Israel kwamba msimuabudu yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na muwatendee wema wazazi wawili...}

(٨)

{وَإِذْ أَخَدْنَا مِيقَاتَنِي إِسْرَائِيلَ لَا تَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ...}

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu akituambia sisi sote: {Na tumemuusia mwanadamu kwa wazazi wake wawili. Mama yake aliubeba ujauzito wake kwa tabu juu ya tabu na kumnyonyesha kwa miaka miwili, na kwamba unishukuru mimi pamoja na wazazi wako na kwangu ni marejeo ya Watu wote}‘

Uislamu umeikata njia ya kuwatetendea uovu wazazi wawili kwa kila anaefikiria kuwafanyia hivyo, baadhi ya vijana wanaweza kujiona kuwa wao ni wafuasi zaidi wa Dini kuliko wazazi wao, na wakafikia kuwakosea kwa maneno au kwa kuwatendea ubaya, basi sisi tunawaambia vijana hawa kwamba: Sheria takatifu ya Uislamu inatuamrisha kuwatendea wema wazazi wawili na kuwa Wema kwa hata kama wao ni makafiri; mpaka asiwe na kisingizio chochote mtu mwenye kuwatendea uovu wazazi wake wawili kwamba hawawezi kuongoka tena.

Na katika jambo hili, anasema Mkweli, Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na ikiwa watakulazimisha kunishirikisha mimi kwa yale usioyajua basi usiwatii. Na uwe nao Duniani kwa wema, na uifuate njia ya wale wanaomtegemea na kuniabudu kisha kwangu mimi ni marejeo yenu nyinyi nitakuambieni yote mliyokuwa mkiyatenda}

Na kutoka kwa Asmaa Binti Abuu Bakar R.A, amesema:

Mama yangu alinijia akiwa mshirikina katika zama za Mtume S.A.W, akitaka niungane nae kiundugu, nikamwomba Mtume S.A.W, anipe Fatwa ya Jambo hili. Nikasema: Ewe Mtume, je niungane undugu na mama yangu? Mtume S.A.W, akamwambia, ndiyo. Unga undugu na mama yako.

(۱)

Kwa hiyo wazazi wawili pamoja na ukafiri wao au hata katika hali ya wao kujaribu kukupeleka kwenye kumuasi Mwenyezi Mungu au hata kutaka kukupeleka katika ukafiri basi usiwatii katika hilo, hata hivyo jambo hilo lisikupelekee wewe kuwatendea ubaya yoyote kati yao. Bali unapaswa kuwa katika hali zako zote kama alivyokuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema:

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na uwe nao Duniani kwa wema}

Na unapaswa kutambua kuwa hakika kufanya hivyo sio fadhili zako bali ni haki na wajibu juu yako na utapata dhambi ikiwa utazembea au kutofanya hivyo.

Kwa hiyo uzuri ulioje kwa yule anayemfanyia wema mama yake na akajitahidi katika kumfanyia wema huo na kufanya bidii ya kumridhisha mama yake. Kutoka kwa Abdullahi bin Amru R.A amesema: Mtume S.A.W, anasema: (Ridhaa ya Mwenyezi Mungu ipo katika ridhaa ya wazazi wawili, kukasirika kwa Mwenyezi Mungu kuko katika kukasirika kwa wazazi wawili).

Ewe Mola wetu tusaidie sisi katika kuwatendea wema wazazi wetu, na uwasemeshe makosa yao na uwarehemu kama walivyotulea sisi tulipokuwa watoto wadogo.